**MKATABA WA KUNUNUA ARDHI, MALIPO YA FIDIA NA MAENDELEO YAKE, HATI YA KUTOWEKA PINGAMIZI (NOC) PAMOJA NA NOTISI YA KUONDOKA KWENYE ARDHI INAYOFIDIWA.**

Makubaliano yamefikiwa leo tarehe 03/05/2025 kati yangu, Bw. **HAJI RASHIDI KUNDA** (ambaye naachia ardhi na maendeleo yake) kwa kampuni ya **CLASSIC MINING COMPANY LIMITED**, iliyosajiliwa chini ya sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (inayochukua ardhi) kama ifuatavyo:

Mimi, Bw. **HAJI RASHIDI KUNDA** ni mmiliki halali wa vipande vya ardhi vilivyopo kitongoji cha Lukowe, katika kijiji cha Mkaranga, wilayani Ruangwa vyenye ukubwa wa ekari 1.93 na 2.72 **(jumla ya ekari 4.66)**

. Ninakubali yafuatayo:-

1. Ninakubali kwa hiari kutoa ardhi yangu iliyotajwa hapo juu kwa Classic Mining Company Limited kwa ajili ya uwekezaji .
2. Nimepokea malipo kamili na ya mwisho ya kuzingatia kwa mauzo ya ardhi iliyotajwa na fidia ya mazao au rasilimali nyinginezo zilizoko kwenye ardhi hiyo kwa jumla ya shilingi za Kitanzania 4,425,621/= ambapo malipo ya fidia ya miti, mazao na gharama ya usumbufu ni kiasi cha shilingi za Kitanzania 3,449,121/= na malipo ya fidia ya ardhi ni kiasi cha shilingi za Kitanzania 976500/= .
3. Kuanzia leo, mimi au familia yangu au mrithi wangu halali au jamaa zangu si wamiliki tena wa ardhi iliyotajwa hapo juu.
4. Nimegawa umiliki pamoja na kila aina ya haki nyingine kwenye ardhi hii na mazao, miti, nyumba au rasilimali nyingine yoyote iliyoko kwenye ardhi hiyo kwa Classic Mining Company Limited kwa hiari yangu, bila kushurutishwa au kulazimishwa na mtu yeyote, na mkurugenzi kwa niaba ya Classic Mining Company Limited amepokea na kukubali umiliki pamoja na kila aina ya haki nyingine kwenye ardhi iliyotajwa hapo juu. Umiliki pamoja na kila aina ya haki nyingine na hatimiliki sasa itakuwa ya Classic Mining Company Limited.
5. Nina haki na umiliki halali wa ardhi iliyotajwa hapo juu. Ninatangaza zaidi kwamba ardhi hii iko wazi, haina vikwazo vyovyote na haina mgogoro wa aina yoyote. Ninawasilisha kwamba sijatia saini / kutekeleza makubaliano yoyote au wosia au zawadi au aina yoyote ya uhamisho au uuzaji au kukodisha na mhusika mwingine yeyote hapo awali kuhusiana na ardhi hii na nina umiliki na kila aina ya haki nyingine zinazohusiana na ardhi hii kuingia/kutekeleza mkataba huu.

6. Endapo kutatokea mgogoro wa aina yoyote unaohusiana na ardhi hii kabla ya tarehe ya makabidhiano au siku zijazo kama vile mgogoro wa mstari wa mpaka, mgogoro wa umiliki, kutoka kwa mtu yeyote au ardhi ikiwa kwa mkopo au makubaliano mengine au mgogoro na serikali, au kodi ya ardhi inayodaiwa na serikali, nitawajibika pekee kusuluhisha mzozo huo na/au kulipa dhima na Classic Mining Company Limited haitawajibika kwa lolote.
7. Endapo nitahitajika nitatoa ushirikiano kwa kampuni ya Classic Mining Company Limited katika kutatua tatizo lolote litakalojitokeza na ardhi hii pasipo gharama yoyote kwa Classic Mining Company Limited na kwamba gharama zozote zitakazotokea wakati wa utatuzi wa mgogoro huo zitakuwa juu yangu.
8. Nimehamisha umiliki pamoja na kila aina ya haki nyingine za ardhi husika kwa Kampuni ya Classic Mining Company Limited na kwamba mara baada ya kusainiwa kwa mkataba huu, sina haki, madai, riba ya mazao, miti, nyumba au rasilimali nyingine yoyote iliyopo, juu ya ardhi hiyo na kwamba mimi au familia yangu au mrithi wangu halali au jamaa zangu, hawatakuwa na haki yoyote ya kuingia au kutumia ardhi hiyo.
9. Nitaacha umiliki wa ardhi hiyo kwa amani na kuikabidhi kwa Classic Mining Company Limited ndani ya siku thelathini (30) zinazoishia tarehe 04/06/2025. Ndani ya siku hizi 30, nitaondoa mali zangu zote zinazohamishika kama vile bidhaa za nyumbani, makaburi, vifaa vya ujenzi n.k na kwamba sitaharibu au kukata miti au mazao yaliyoko/yanayopatikana kwenye ardhi hiyo. Baada ya siku thelathini, Classic Mining Company Limited itamiliki ardhi iliyotajwa na milki hiyo halali itachukuliwa kuwa katika jina la Classic Mining Company Limited. Nimekabidhi umiliki wa ardhi hiyo kwa Classic Mining Company Limited na Classic Mining Company Limited imechukua milki ya ardhi hiyo.
10. Iwapo kuna mgogoro wowote, nitajaribu kuusuluhisha kwa maridhiano au ikibidi, Classic Mining Company Limited na mimi tutateua msuluhishi ambaye ni pamoja na Afisa Tawala wa Wilaya (DAS) na Afisa Mtendaji wa Kata. Hata hivyo, Classic Mining Company Limited itakuwa na haki ya kwenda mahakamani.
11. Nimeelewa mkataba huu na kwa hiari yangu, bila kushurutishwa au kulazimishwa na mtu yeyote, nakubali kutia saini kukubali malipo ya kuzingatia mauzo na fidia ya ardhi.



**Imesainiwa mbele ya-**

1. Classic Mining Company Limited (Mlipaji)

   Jina la Mkurugenzi: Mahendra Bardiya

   Sahihi: [signature]

   Tarehe: 03/05/25.

2. Jina la mpokeaji: **HAJI RASHIDI KUNDA**

   Sahihi ya dole gumba: * [thumbprint]

   Tarehe: 03/05/2025

**Imeshuhudiwa na:**

1. **Afisa Mtendaji wa Serikali** ya Kijiji cha MKARANGA

   Jina JANE JULIUS NYITARA Sahihi [signature] Tarehe 03/05/2025.

2. **Classic Mining Company Limited, (mwakilishi)**

   Jina MOHAMED FUNDI Sahihi [signature] Tarehe 03/05/2025

# HAJI RASHID KUNDA

5th April 2025

New Surveyed Road to QV2 (813.5m)




Nambilanje – Ruangwa road.

**MALIPO YA ARDHI NA MAENDELEO YAKE**

Mimi, **HAJI RASHIDI KUNDA** mmiliki wa vipande vya ardhi vilivyopo katika kitongoji cha Lukowe katika kijiji cha Mkaranga, kata ya Nambilanje,wilayani Ruangwa, vyenye ukubwa wa ekari 01.93 na 2.72 **(jumla ya ekari 4.65)** ~~nathibitisha kupokea hundi namba~~ Taslimu ~~yenye~~ kiasi cha shilingi za kitanzania 4,425,621 /=, ambapo malipo ya fidia ya miti, mazao pamoja na gharama ya usumbufu ni shilingi za kitanzania 3,449,121 /= na malipo ya fidia ya kiasi cha ardhi ni shilingi za kitanzania 976500 /=

Sahihi ya Mpokeaji/mlipwaji ______________ tarehe 03/05/2025 kidole gumba X

Sahihi ya Mtoaji/mlipaji ______________ tarehe 03/05/2025

**Shahidi wa mlipwaji**

1. Jina YUSUPH M. MAWALA Sahihi ______________ tarehe 03/05/2025
2. Jina SHARAFA B. MBOGA Sahihi S.B. Mboga tarehe 03/05/2025

**Shahidi wa mlipaji**

1. Jina MOHAMED FUNDI Sahihi ______________ tarehe 03/05/2025
2. Jina HARIPAL MEENA Sahihi ______________ tarehe 03/05/2025

| S/N | Name of Owner | Initials | Plot size | Land rate per acre (Tshs) | Price of Plot (Tshs) | Disturbance allowance 5% | Land Value of Plot Tshs | Type of crops and quantity/stem | Qty/acre | Growth Stage | Price of crop per acre /stem (Tshs) | Value of crop/and or Land Price (Tshs) | Value of Crop and or Land Tshs | Amount Payable (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | HAJI RASHDI KUNDA | HRK | 4.65 | 200,000 | 930,000 | 46,500 | 976,500 | Cashewnuts | 13 | 100 | 223,332 | 2,903,316 | 3. | 4,425,621 |
| | | | | | | | | Sugarcane | 3 | 100 | 2,617 | 7,851 | | |
| | | | | | | | | bananas | 6 | 100 | 47,209 ~~5,677~~ | 283,254 | | |
| | | | | | | | | Coconut | 1 | 100 | 255,000 | 255,000 | | |